

MCHANGO WA LUGHA YA KISWAHILI KATIKA KUKUZA UZALENDU NCHINI TANZANIA

Stella Faustine
Chuo Kikuu cha Dodoma – Tanzania
stelafau@gmail.com

Ikisiri

Uzalendo ni dhana inayofafanua hali ya mtu kuwa na mapenzi na nchi yake; na hivyo, kuipa thamani. Katika mijadala ya kitaaluma, watafiti mbalimbali kama vile Bar na Amos (2004) na Yonah (1999), wamejadili namna uzalendo unavyoweza kukuzwa katika jamii kwa kuunasibisha moja kwa moja na mapenzi ya mtu binafsi kwa taifa lake pasipo kuunasibisha moja kwa moja na lugha ya Kiswahili kama sehemu ya utamaduni wa taifa na pia nyenzo kuu ya mawasiliano. Jambo hili linasababisha nafasi ya Kiswahili kutopewa umuhimu wake kama nyenzo madhubuti inavyoweza kutumika kama njia ya kukuza uzalendo kwa jamii; na kuchochea maendeleo ya taifa. Makala imekusudiwa kuziba pengo hilo kwa kuonesha namna lugha ya Kiswahili inavyoweza kukuza na kuendeleza uzalendo hususani nchini Tanzania. Utafiti uliozalisha makala hii umejikita katika mwegamo wa kitaamuli. Data mbalimbali zinazohusiana na mada ya utafiti zilipatikana maktabani kwa kutumia mbinu ya udurusu wa nyaraka. Vitabu teule vya 'Babu Alipofufuka', 'Nagona' na 'Nyerere na Safari ya Kaanani' vimetumiwa kutoa mifano ili kushadidia hoja za msingi. Pia, wimbo wa 'Tanzania, Tanzania' umetumika kutoa mifano hiyo. Mjadala uliongozwa na Nadharia ya Sosholojia ambayo inahusu uchunguzi wa jamii katika masuala mbalimbali ya kiuchumi, kisiasa na kiutamaduni. Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa lugha ya Kiswahili ina mchango mkubwa katika kukuza uzalendo nchini Tanzania kwa kutoa mafunzo mbalimbali kwa njia ya mawasiliano ambayo huwaunganisha watu na kuwafanya wamoja. Pia, kupitia tanzu za fasihi, hutumika kutoa mafunzo mbalimbali yanayokusudiwa kumjenga, kumwelimisha, kumwonya na kumhamasisha mwanajamii kuhusu masuala mbalimbali yanayomfanya kuishi kwa kufuata misingi na itikadi za jamii yake.

1.0 Utangulizi

Mara nyingi tumekuwa tukiyasikia baadhi ya maneno katika maeneo mbalimbali ama ya kitaaluma au katika mazingira yanayotuzunguka pasipo kuyatilia maanani. Kupuuuzwa kwa maneno hayo kunaweza kuleta hasara au kuchelewesha mtu, watu au jamii kufikia malengo yanayotarajiwa. Si tu katika kuyatilia maanani maneno hayo, bali hata katika kuelewa uzito wake. Uelewa sahihi ndio msingi wa utekelezaji makini, madhubuti na pia wenye tija kwa jamii. Huwezi ukaambiwa ongea na ukaanza kuongea pasipo kuelewa umeambiwa uongee nini. Kuongea pasipo kuelewa umekusudia kuongea nini, kunaweza kusababisha kuongea yasiyo sahihi; na hivyo, kuvuruga mawasiliano ambayo ndiyo chanzo cha utekelezaji wa lililokusudiwa kuongelewa.

Hitaji la mawasiliano yenye kueleweka linazua chachu ya kutaka kuelewa maana ya uzalendo. Uelewa huu ndio utakaosaidia kuinasibisha lugha ya Kiswahili katika kukuza na kuendeleza uzalendo miongoni mwa wanajamii nchini Tanzania.

1.1 Uzalendo

Uzalendo ni dhana ambayo imekuwa ikihusishwa na maendeleo ya jamii; kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni. Akifafanua kuhusu maana ya uzalendo, Yonah (1999) anatuambia kuwa ni aina ya upendo na uaminifu wa mtu anaouhisi kwa watu wenzake au nchi yake, ni uaminifu utokanao na tamaa ya ndani badala ya utambuzi. Anaendelea kufafanua kuwa uzalendo ni msukumo asili ambao mtu anazaliwa na kukua nao unaobainisha upendo wa dhati katika kukuza na kumthamini mtu, jambo, kitu au nchi yake. Maana sawa na inayotolewa na Yonah (*khj*), inafafanuliwa na Bar na Amos (2004). Hawa, wanaeleza maana ya uzalendo katika ujumuifu kwa kusema kuwa ni uhusiano baina ya mtu binafsi, taifa lake na nchi anayoishi.

Kwa upande wa BAKIZA (2010), wanafafanua uzalendo katika mitazamo miwili; wa kwanza ni mtazamo finyu ambao unaeleza kuwa uzalendo ni:

- i. Hali ya mtu kuwa na nasabu ya asili ya nchi

Hii inamaanisha kuwa, ili mtu awe mzalendo katika taifa fulani, ni lazima awe na uhusiano wa ki-asili wa kuzaliwa katika taifa hilo. Mtazamo wa pili ni ule unaoifafanua dhana ya uzalendo kwa mapana kwa kuihusisha nasabu ya asili ya mtu pamoja na mapenzi ya dhati aliyonayo katika kuitumikia, kuitetea na kuilinda nchi yake. Katika mtazamo huu, wanafafanua kuwa ni:

- ii. Hali ya mtu kujitolea kwa hali na mali kwa ajili ya nchi yake

Aidha, maana ya pili inaonesha wazi kuwa upo uhusiano mkubwa kati ya dhana ya uzalendo na mapenzi ya mtu binafsi kwa jamii yake. Maana hii inashadidiwa na maana inayotolewa na TUKI (2004) ambao mwanaongeza kipengele cha kujitolea muhanga kama kipengele muhimu kinachoashiria uzalendo wa mtu kwa nchi yake. Wanasema kuwa uzalendo ni hali au fikra ya mtu kuwa tayari kufa kwa ajili ya uhuru na usalama wa nchi yake. Fasili zinazotolewa na wataalamu waliotajwa hapo awali, zinajenga tafakuri ambayo inazua maswali kadhaa. Miongoni mwayo ni: je, mzalendo ni nani? au je, uzalendo unaanzia wapi?

Kimsingi, kama ambavyo inaelezwa na BAKITA (2017), mzalendo ni mtu mwenye asili ya mahali fulani kwa kuzaliwa. Mwenye kuipenda nchi yake kwa moyo wake wote, kwa kiasi cha kuwa tayari kuipigania. Mara nyingi watu wamekuwa wakidhani kuwa uzalendo ni wa mtu na taifa lake. Wamekuwa wakijiwekea mipaka ya utekelezaji na kushindwa kutekeleza majukumu katika ngazi mbalimbali, jambo ambalo linasababisha kushindwa kufikia malengo. Kwa jumla, uzalendo huanzia kwa mtu binafsi. Katika nafasi yake lazima mtu ajitambue na ajithamini ndipo aweze kutoka nje ya mipaka ya uyeye. Baada ya hapo, mtu huyu ataweza kuipenda familia yake. Kijana au mtu yeyote hana budi kuithamini familia yake kwa kuwa na nidhamu ya hali ya juu. Utamaduni wa kudumisha nidhamu ukianza katika mazingira ya nyumbani, mtu/kijana bila shaka, atakuwa na nidhamu shuleni, katika mazingira yanayomzunguka na hatimaye kwa taifa zima. Mtu katika nafasi yake hawezi kuwa raia mwema ikiwa atakiuka maadili yaliyowekwa kwa misingi ya utamaduni wa jamii yake. Mila na desturi zinazojengwa katika tamaduni zetu ni nguzo zinazomfinyanga raia mwema. Yote haya yatafikiwa kama mtu atakuwa na mapenzi ya dhiti na misingi ya kimaadili ya jamii yake. Katika muktadha huu hapa tunakuwa na viwango vitatu vya uzalendo, kama:

- i. Uzalendo wa mtu binafsi;
- ii. Uzalendo kwa mtu na mtu; na
- iii. Uzalendo kwa mtu na nchi/taifa lake.

Mtu akiishi katika misingi ya uzalendo ataitambua thamani yake. Kwa hakika ni muhimu kuelewa kuwa vipo viashiria kadhaa ambavyo vinaubainisha uzalendo wa mtu; aidha kwake binafsi, kwa mtu na mtu au kwa taifa. Viashiria hivyo kama ambavyo vimegusiwa na Yonah (1999),

Bar na Amos (2004), TUKI (2004) na BAKIZA (2010) kwa kutaja wachache, ni upendo ambao kimsingi unajidhihirisha kupitia:

- i. Uaminifu anaoujenga mtu kwake binafsi, kwa mtu na mtu na kwa taifa lake;
- ii. Utayari wa kujitoa kwa lolote katika kutetea masilahi ya mtu au taifa kwa gharama yoyote;
- iii. Nidhamu na utii kwa mtu na mtu na kwa taifa (hii inajumuisha utii wa sheria bila shuruti);
- iv. Kuwa na umoja na ushirikiano kwa ajili ya masilahi mapana ya mtu/watu na taifa kwa jumla;
- v. Kuwa balozi na mlinzi mzuri wa rasilimali za taifa;
- vi. Kuwa na bidii katika kufanya kazi kwa masilahi mapana ya taifa;
- vii. Kuthamini, kulinda na kuzitunza alama ya taifa kama sehemu ya kuulinda utaifa wetu;
- viii. Kuthamini, kulinda na kuheshimu utamaduni wa jamii au taifa husika; na
- ix. Kuishi katika misingi ya haki, usawa, na kuthamini utu wa binadamu.

Kwa ujumla, maelezo ya wataalamu tajwa hapo juu yanadhihirisha kuwa mwimo wa ujenzi na utekelezaji wa dhana nzima ya uzalendo ni upendo. Pasipo kupingana na maelezo ya wataalamu hawa, makala hii inaibua swali la msingi kuhusu nafasi ya lugha katika nyanja ya kimawasiliano katika kuujenga uzalendo. Hoja kuu inajengwa katika msingi kuwa, je upendo ambao unakitwa katika kujenga uzalendo unaweza kutekelezeka pasipo mawasiliano ambayo hufanywa kwa njia ya lugha?. Kimsingi, swali hili ndilo linalojibiwa na makala hii kwa kuonesha namna lugha ya Kiswahili kupitia nyanja mbalimbali, inavyochangia kukuza uzalendo nchini Tanzania.

2.0 Kiunzi cha Nadharia

Uchambuzi na uwasilishaji wa data zilizoalisha makala hii uliongozwa na Nadharia ya Sosholojia. Scott (1999) na Cross (2011) wanabainisha kuwa sosholojia ni nadharia inayohusu uchunguzi wa jamii katika masuala mbalimbali ya kijamii, kisiasa na kiutamaduni. Kwa mantiki hiyo, lugha ya Kiswahili kama sehemu ya utamaduni wa jamii, nayo hujifungamanisha na jamii husika katika kutekeleza masuala mbalimbali ya kimawasiliano na hivyo kuchochea maendeleo ya jamii. Kutokana na uhusiano huo, Nadharia ya Sosholojia ilisaidia kupata taarifa mbalimbali

ambazo zilizalisha makala hii kwa kumakinikia umuhimu wa mawasiliano na uchangamani wake kimawasiliano katika jamii.

Kwa upande mwingine, nadharia hii ilisaidia katika kubainisha namna kazi za fasihi ya Kiswahili kama nyanja mojawapo ya utamaduni inavyoweza kuchangia katika kukuza na kuendeleza uzalendo katika mukatadha wa kimawasiliano. Hii ni kwa sababu, lugha ndiyo malighafi muhimu katika kujenga kazi ya fasihi. Kwa maana hiyo, uwasilishwaji wa maudhui ndani ya kazi za fasihi ya Kiswahili haziwezi kujitenga na lugha ya Kiswahili. Njogu na Chimera (1999) wanaelezea kuwa Nadharia ya Sosholojia inaifungamanisha fasihi na jamii. Inaonesha kuwa sosholojia ni kielelezo cha hali halisi ya jamii na inachukuliwa kama zana mojawapo ya kijamii dhidi ya mazingira makali. Wanaendelea kueleza kuwa nadharia hii inasisitiza kuwa fasihi ni amali ya jamii. Kwa misingi hiyo, huweza kutumia lugha katika kuwasilisha masuala mbalimbali ya kijamii kwa lengo la kufunza, kuonya, kuadilisha na kuhifadhi amali za jamii husika.

3.0 Methodolojia ya Utafiti

Utafiti huu ni wa kimaktaba. Data zilikusanywa kwa kutumia mbinu ya udurusu wa nyaraka ambayo ni mbinu ya kukusanya data kutoka kwenye vyanzo mbalimbali vya maandishi (Kothari, 2004). Mbinu hii humpa mtafiti undani wa masuala yanayotafitiwa kwa kuyalinganisha na ama kuyapatanisha na ushahidi kutoka katika vyanzo vya awali. Mtafiti alitumia mwongozo wa udurusu katika kusoma matini teule zilizohusiana na mada husika. Pia, mbinu ya udurusu wa nyaraka ilimwongoza mtafiti kusoma vitabu na kudurusu nyimbo mbalimbali za fasihi ya Kiswahili ili kubaini ni kwa namna gani vinaweza kuchangia kukuza uzalendo. Data hizi zilichanganuliwa na kuwasilishwa kwa kutumia mkabala wa kitaamuli ambao unatumia mbinu ya kimaielezo. Aidha, vitabu teule vya nathari, yaani *Babu Alipofufuka*, *Nagona* na *Nyerere na Safari ya Kaanani* zimetumiwa kutoa mifano ili kushadidia hoja za msingi. Pia, wimbo wa *Tanzania, Tanzania* umetumika kutoa mifano hiyo. Zote hizi zimetumiwa kama sehemu tu ya kuwakilisha kazi nyingine za fasihi.

4.0 Kiswahili katika Kujenga Uzalendo: Mukatadha wa Kimawasiliano

Ili taifa liweze kuwa imara na madhubuti katika nyanja tatu, yaani uchumi, siasa na utamaduni kwa kujikita katika utekelezaji wa misingi ya uzalendo, lazima tuwe na lugha madhubuti ambayo kupitia kwayo,

maarifa na misingi kuhusu dhana ya uzalendo inaweza kuwasilishwa kutoka kwa mtu mmoja na mwingine.

Nchini Tanzania, Kiswahili ndiyo lugha inayoeleweka kwa Watanzania walio wengi (Sewangi, 2004); na hivyo, inafaa kuwa ni chombo cha kuwaunganisha watu na kuwafunza mambo mbalimbali kuhusu mustakabali wa taifa lao katika masuala ya kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni. Mafunzo haya huwajengea wananchi moyo wa upendo miongoni mwao, huwaleta pamoja na kuwa wamoja; na hatimaye, kuwa wazalendo katika taifa. Kwa mfano, nchini Tanzania, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere aliweza kuwafunza wananchi masuala mbalimbali yaliyowajengea moyo wa uzalendo kupitia hotuba zake alizozitoa kwa kutumia lugha ya Kiswahili. Katika moja ya hotuba hizo, aliwasisitiza wananchi kuhusu kuwa na umoja na mshikamano ambao utawafanya kuwa ndugu moja. Alisema:

Umoja na mshikamano ndio silaha ya kupambana na dhuluma na unyonyaji

tujenge misingi ya umoja ili tuelewane na tujuane kuwa ni wamoja na ndugu,

(Liundi, 2015: 36-37)

Anachokisisitiza Mwalimu Julius Kambarage Nyerere hapa, ni umoja na mshikamano miongoni mwa wananchi. Yamkini, hotuba hii ingeandikwa kwa lugha nyingine tofauti na lugha ya Kiswahili, Watanzania ambao ni watumiaji wa lugha ya Kiswahili, wasingeweza kuelewa na kufanya utekelezaji wa masuala muhimu yanayoongelewa katika hotuba hiyo ambayo inalenga kujenga uzalendo kwa manufaa ya taifa. Kwa mantiki hiyo, kama Nadharia ya Sosholojia inavyotuelekeza kuwa utamaduni wa jamii lazima ujifungamanishe na muktadha wa jamii husika, lugha kama sehemu ya jamii hiyo imeweza kuwaunganisha wanajamii na kuwa wamoja kutokana na kuwa na utamaduni wa aina moja unaosawiriwa kupitia lugha zao.

Halikadhalika, lugha ya Kiswahili ina nafasi kubwa katika kujenga uzalendo kwani hutumika kama njia ya mawasiliano katika kutekeleza majukumu mbalimbali kama vile kutoa elimu kwa Watanzania kuhusu masuala mbalimbali ya kitaifa. BAKITA (2017) wanafafanua hili kwa kusema kuwa nchini Tanzania, Kiswahili ndiyo lugha rasmi inayotumika kutolea elimu katika ngazi mbalimbali za elimu ya msingi na elimu ya juu. Pia, ni lugha mwafaka katika kutoa mafunzo mbalimbali makanisani, misikitini, katika televisheni na mitandao ya kijamii yenye lengo la kujenga uzalendo kwa wanajamii. Hii ni kwa sababu, kama ambavyo

imekwishaelezwa hapo awali, ndiyo lugha inayofahamika kwa Watanzania walio wengi na imezidi kukua na kupanuka kila kukicha.

Suala la uzalendo limekuwa likijadiliwa katika maeneo mbalimbali. Moja ya maeneo hayo ni shuleni ambapo mijadala hiyo imekuwa ikitolewa kama elimu ya msingi katika kuwaandaa vijana kulitumikia taifa lao. Ikumbukwe kuwa teknolojia makini inapatikana kwa elimu sahihi na elimu sahihi hupatikana kwa lugha yenye kueleweka baina ya pande zote mbili. Maelewano haya ambayo yanatokana na lugha sahihi inayoeleweka kati ya mfunzaji na mjifunzaji, humwezesha mjifunzaji kunyonya maarifa anayopewa kwa urahisi na hivyo kumjengea moyo wa upendo, kuthamini na kujitoa katika kutekeleza majukumu ya kitaifa. Umuhimu wa matumizi ya lugha ya Kiswahili kama lugha mwafaka katika kutoa maarifa kwa wazungumzaji wake, umeelezwa na Shaaban Robert mnamo mwaka 1954. Alipoulizwa kuhusu uamuzi wa kuandika kazi zake kwa lugha ya Kiswahili, alisema:

Labda maandiko bora kuliko ya kalamu yangu nyonge yamekwisha kuwa katika Afrika Mashariki. Lakini mashaka ya lugha zake ngeni si madogo. Yawalazimu wenyeji kunyonya kwa taabu maarifa yake kama watoto walishwao kwa chupa badala ya matiti ya mama zao. Maandiko yangu yatakuwa katika lugha moja kubwa ya Afrika Mashariki. Kwa kufanya hivi, watu wengi wataweza kunyonya kwa matiti waliyozoea. Hivyo, nitafanya sehemu yangu ndogo ya msaada katika maendeleo ya nchi yangu (Senkoro, 1995: 61).

Nukuu hii inathibitisha ugumu na mashaka ya kunyonya maarifa ya kitaaluma kwa kutumia lugha ngeni. Utambuzi huu unaipa nafasi kubwa lugha ya Kiswahili kama lugha ya kimawasiliano katika kutoa mafunzo kwa vijana kuhusu umuhimu wa kuwa wazalendo kwa masilahi mapana ya taifa lao. Nchini Tanzania, katika shule za msingi, mathalani, vijana wamekuwa wakifundishwa somo la uraia kwa kutumia lugha ya Kiswahili wanayoielewa vyema; na hivyo, kukuza ari ya uzalendo ndani yao. Mfano mzuri ni elimu wanayoipata darasa la saba ambayo inawapa misingi na utambuzi wa kuzielewa haki za binadamu, misingi ya mahakama na mhimili wa bunge. Elimu hii inawasaidia kuwa raia wazalendo wanaoishi kwa kuzingatia haki, sheria na misingi ya taifa lao pasipo kukiuka; na hivyo, kuvuruga amani ya taifa.

Watafiti na wataalamu mbalimbali wamekuwa wakiandika masuala mbalimbali ya kiuchumi, kisiasa na kitamaduni kwa kutumia lugha ya

Kiswahili. Maandiko yao yamekuwa na msaada mkubwa katika kutoa uelewa kwa wanajamii kuhusu taifa lao na mustakabali wake. Hii ni kwa sababu maandiko hayo yameandikwa kwa kutumia lugha ya Kiswahili ambayo inaeleweka kwa Watanzania wengi. Miongoni mwa vitabu vilivyoandikwa kutokana na tafiti hizo ni: REDET (2005) kikieleza kuhusu ujenzi wa imani ya jamii na amani Tanzania. Kitabu hiki kinawafanya wanajamii kuelewa umuhimu wa amani kwa taifa lao na hivyo kuwa tayari kuilinda na kulitumikia taifa lao kwa hali na mali. Kasembo (2012) aliandika kuhusu tathmini ya miaka hamsini ya uhuru: tulikotoka, tulipo na tunakokwenda. Andiko hili linawajenga wananchi kutathmini maisha yao kabla na baada ya ukoloni na hivyo kuwajengea misingi ya kulilinda, kuliheshimu na kuuthamini uhuru wao ambao waliupigania kwa hali na mali. Naye Mwandosya (2013) anaeleza kuhusu udhibiti na huduma za kiuchumi Tanzania. Kwa ujumla, ndani ya maandiko haya, kuna masoala mbalimbali ambayo yanajenga jamii na kuifanya kuwa na hali ya kulithamini, kulitetea, na kulinda taifa na rasilimali zake kwa masilahi mapana ya taifa.

5.0 Fasihi ya Kiswahili katika Kujenga Uzalendo

Dhana ya uzalendo inakwenda sambamba na hali au matakwa ya wanajamii kuelewa jamii yao pamoja na misingi ya jamii hiyo. Kama anavyoeleza Simala (2017), mawasiliano katika jamii ni msingi mzuri wa kurejelewa ili kuelewa jamii husika. Hii ni kwa sababu lugha hubeba maana, nayo maana ndiyo msingi wa mawasiliano na mawasiliano ndiyo msingi sahihi katika kujenga na kukuza uzalendo. Nchini Tanzania, misingi ya kimawasiliano hufanyika na kudhihirika pia kupitia tanzu mbalimbali za fasihi ya Kiswahili. Hii inatokana na kile anachokieleza Mulokozi (2017), kuwa kitambulisho kikubwa cha fasihi ya Kiswahili ni lugha ya Kiswahili ambayo hutumika kama nyenzo ya kimawasiliano katika kuwasilisha maudhui kwa jamii. Miongoni mwa tanzu hizo ni zile za nudhumu, nathari pamoja na semi mbalimbali. Hizi, kwa kutumia lugha ya Kiswahili hutoa mafunzo mbalimbali yaliyokusudiwa kumjenga, kumwelimisha, kumwonya na kumhamasisha mwanajamii kuhusu masuala mbalimbali yanayomfanya kuishi kwa kufuata misingi na itikadi za jamii yake.

5.1 Nudhumu

Nudhumu ni tungo za kishairi ambazo aghalabu huzingatia matumizi ya lugha ya mkato, au ya kishairi. Miongoni mwa tungo hizo ni nyimbo ambazo kwa muda mrefu hutumiwa na jamii mbalimbali katika malezi na makuzi ya watoto. Awali, kabla ya ujio wa wakoloni jamii ya Waswahili ilitumia nyimbo kama darasa la kutolea mafunzo mbalimbali yenye lengo

la kuhakikisha vijana wanakuwa katika maadili yenye kufuata misingi bora. Pia, zilitumika kama silaha ya kuwatia watu moyo na kuwafanya wamoja katika utelelezaji wa shughuli za kijamii (Senkoro, 1987). Simiyu (2011) anatueleza kuwa nyimbo husheheni mawazo mazito ambayo kwayo, jamii hujifunza mambo mbalimbali.

Kama Nadharia ya Sosholojia inavyotuelekeza kuwa fasihi ni amali ya jamii hivyo huweza kutumia lugha katika kuwasilisha masuala mbalimbali ya kijamii, nyimbo kama utanzu mmojawapo unaotumia lugha huweza kutumika kama darasa la kutoa mafunzo mbalimbali yanayojenga uzalendo kwa wanajamii. Nchini Tanzania, nyimbo huimbwa katika maeneo mbalimbali; ambayo ni rasmi, kwa mfano, shuleni na halaiki za kitaifa pamoja na yale yasiyo rasmi. Kwa mfano, wimbo wa ‘Tanzania Tanzania’ kama ambavyo umenukuliwa na Simiyu (2011), mara nyingi huimbwa katika shule za msingi kwa kuisifia nchi ya Tanzania; na hivyo, kutangaza thamani na fahari yake. Hii huwafanya vijana kuipenda kuithamini na kuilinda nchi yao kwa moyo wa dhati. Maneno ya wimbo huo ni kama yafuatayo:

Tanzania Tanzania

*Tanzania Tanzania,
Nakupenda kwa moyo wote,
Nchi yangu Tanzania,
Jina lako ni tamu sana,
Nilalapo nakuota wewe,
Niamkapo ni heri mama we!
Tanzania Tanzania,
Nakupenda kwa moyo wote.*

*Tanzania Tanzania,
Ninapokwenda safarini,
Kutazama maajabu,
Biashara nayo makazi,
Sitaweza kusahau mimi,
Mambo mema ya kwetu kabisa,
Tanzania Tanzania,
Nakupenda kwa moyo wote...*

Wimbo huu uimbwapo, humfanya msikilizaji kujua thamani na fahari ya Tanzania lakini pia wema na ukarimu wa Watanzania kama

unavyoelezwa katika ubeti wa pili, na hivyo, kujenga mapenzi juu ya nchi pamoja na watu wake.

5.2 Nathari

Dhima ya lugha ya Kiswahili katika kuujenga uzalendo inakwenda sambamba na kuelimisha jamii kuhusu maadili na mielekeo sahihi kwa jamii. Kutokana na wimbi la utandawazi ambalo limeifanya dunia kuwa kama kijiji, kumekuwapo na mwingiliano wa tamaduni kutoka katika mataifa ya Kimagharibi. Jambo hili limewafanya vijana kudharau misingi mila na desturi za taifa lao, na hivyo, kupoteza uzalendo wa kuthamini mila, desturi na tamaduni za taifa lao. Mohamed (2001) kupitia utanzu wa riwaya ambao ni moja ya tanzu zinazokitwa katika kumbo za kinathari, anatumia lugha ya Kiswahili kuwajengea vijana uzalendo wa kuthamini umuhimu wa kuwa na maadili mema katika jamii. Katika riwaya ya *Babu Alipofufuka*, anatumia lugha fasaha ya Kiswahili kumuasa mjukuu wake K. kuwa kila jamii ina taratibu zake zinazopaswa kufuatwa na kuheshimiwa. Anasema:

Kila kitu kimeumbwa na kanuni zake K na kwa hiyo,
huwezi kung'oa *mmbilimbi* Pemba na kwenda
kuupandikiza Montreal. Hauwi ng'o, hauwi! na hata
ukiduhushiwa na kudekezwa vipi kwenye vitalu,
hauwezi kuja juu sawasawa na ule wa Pemba.
Pamoja na hayo, utashi wa mwanadamu
umebadilisha kila kitu (uk. 50.)

Kimsingi, nukuu hii inamjenga mtu kuthamini, kuheshimu na hatimaye kuipenda asili yake. Mapenzi haya, ndiyo yanayomfanya mtu kuwa mzalendo wa taifa au jamii yake na hivyo kumfanya aishi kwa kufuata misingi sahihi ya kijamii.

Kwa upande mwingine, lugha ni dafina au ghala la kuhifadhia amali mbalimbali za jamii. Mwandishi yeyote yule anapotaka kuandika jambo fulani kuhusu jamii au suala lolote kwa ajili ya ustawi wa jamii lazima atumie lugha. Katika jamii ya Watanzania, lugha ya Kiswahili imekuwa ikitumiwa kwa namna mbalimbali kama njia ya kuweka kumbukumbu kuhusiana na masuala mbalimbali ya taifa. Akifafanua kuhusu kazi za riwaya ambazo zinatumia lugha ya Kiswahili kutunza kumbukumbu za jamii, Madumulla (2009:20), anatueleza:

...riwaya ya Kiswahili ni dafina kwa hakika,
riwaya zote za kinyaraka na kihistoria kama vile
Bwana Myombekere na Bibi Bugonoka (A.

Kitereza), *Kaburi Bila Msalaba* (P. M Kareithi), *Mzishi wa Baba Ana Radhi*, (F. Nkwera)..., Ni mifano mizuri ya kazi za fasihi zinazosawiri vizuri matukio ya kihistoria, na kutunza historia ya jamii zinazohusika.

Kumbukumbu hizo, zina nafasi kubwa ya kutoa mafunzo kwa jamii na kuwafanya vijana kujenga moyo wa uzalendo kutokana na mambo wanayojifunza kuhusu falsafa, itikadi, mila na desturi za jamii yao na kuwafanya kuishi katika misingi sahihi kulingana na idili za jamii.

Naye Kezilahabi (1990), anatumia lugha ya Kiswahili katika kuwajenga wanajamii kuwa wazalendo kwa kuthamini mali pamoja na rasilimali za taifa lao. Anatimiza jukumu hili kwa kufichua maovu mbalimbali yanayofanywa na viongozi au watu wenye uchu wanaotumia nafasi zao kulihujumu taifa. Katika riwaya hiyo, anaonesha namna miradi mingi ya kitaifa inavyotumika kulihujumu taifa. Kila mwaka, inapangiwa bajeti ya kutafiti masuala mbalimbali lakini mipangokazi haitekelezeki. Anasema:

Tuliandika ripoti yetu na kuikabidhi serikalini. Baada ya miaka kadhaa tulisikia kuwa wataalamu wengine walikuwa wamekuja kufanya utafiti ule ule tuliotumwa kufanya, na kwamba wangelipwa mamilioni ya pesa (uk. 41.)

Nukuu hii inadhihirisha wazi namna fedha za serikali zinavyofujwa kwa manufaa ya watu binafsi. Kazi hii inawafungua macho raia katika kujua maovu mbalimbali yanayotendeka katika jamii na hivyo kujenga hali na moyo wa kuzipigania na kuzilinda rasilimali mbalimbali za taifa.

Kwa upande wa tamthiliya kama utanzu mwingine wa kinudhumu, Mbogo (2015) anatumia lugha ya Kiswahili kueleza kisa cha mwaka 1966 kuhusu vijana wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, waliogoma kujiunga na Jeshi la Kujenga Taifa. Katika kuukabili upinzani huo, Mwalimu anatumia hotuba yake kupenyeza usemi wa Kiswahili: Tanzania itajengwa na wenye moyo, (uk. 53) ambao una dhima ya kujenga uzalendo na kuwapa vijana ari na moyo wa kuwa tayari kulitumikia taifa lao. Anaendelea kusema:

Tanzania haitajengwa na ubinafsi; haitajengwa kwa choyo; haitajengwa kwa tamaa ya kujilimbikizia mali..., Wananchi, Tanzania itajengwa na wazalendo wenye moyo wa kujenga Tanzania (uk. 54.)

Naye, Mohamed (1990) anawafunza vijana kuhusu umuhimu wa kuwa wazalendo kwa kujitoa muhanga ili kupigania masilahi yao binafsi na taifa kwa jumla. Anamtumia Mtolewa ambaye licha ya ukatili wa Bi. Kirembwe, anaingia Giningi na kuwakomboa wananchi waliokuwa chini ya utawala dhalimu wa Bi. Kirembwe. Hii inadhihirika pale Mtolewa anapoeleza azma yake ya ukombozi kwa kusema:

Ishara zimebainika katika upepo wenye nguvu za kupeperusha matamano ya kijinga; upepo wenye nguvu za kufagia; upepo wenye nguvu za kufagia takataka za mawazo mapotofu ili ukweli uonekane baada ya uongo kuwekwa uchi mbele yetu, na bundi mwenye kulia usiku baada ya kuona mengi kwa hiyo niruhusini nifungue mkebe huu ili nitoe unga wa rutuba (uk. 100).

Kimsingi, mafunzo haya ni muhimu kwani huwajengea vijana moyo wa utayari na uaminifu katika kuitumikia jamii yao.

5.3 Semi

Zipo semi mbalimbali za Kiswahili ambazo zinatumiwa katika kukuza uzalendo na utaifa kwa jamii kutokana na maarifa na mafunzo yanayopatikana ndani yake. Miongoni mwazo ni methali, nahau na vitendawili.

Tukichukua mifano kutoka katika utanzu wa methali, hizi ni semi ambazo hutumia taswira na ishara katika kueleza masuala yaliyobeba fikra nzito zinazosawiri masuala ya kifalsafa ya jamii husika. Hutumika katika kutoa miongozo na kufunza maadili katika jamii. Miongoni mwazo ni kama zinavyotajwa na Abdulhamid na Barua (2006):

1. 'Kinga na kinga ndipo moto huwaka' (uk. 20)
2. 'Kufa kwa wengi ni harusi (uk. 21)
3. 'Jifya moja haliinjiki chungu' (uk. 16)

Wanasosholojia wanaamini kuwa upo uhusiano mkubwa kati ya fasihi na jamii na kuwa fasihi ni akisio la yale yanayotokea katika jamii. Kutokana na uhusiano huo, methali kama utanzu wa fasihi ambao huakisi utamaduni wa jamii husika hutumika kutoa mafunzo mbalimbali kwa jamii. Kwa mfano, methali zilizotajwa hapo juu hutoa mafunzo kwa jamii kuwa umoja na mshikamano ni nguzo msingi katika kufanikisha mambo mbalimbali yenye tija katika maendeleo ya taifa. Methali ya 'kinga na

kinga ndipo moto huwa' inahimiza watu wafanye kazi kwa kushirikiana ili waweze kupata mafanikio. Aidha, ile isemayo 'kufa kwa wengi ni harusi' inatia watu moyo na kwa kuwaonesha kuwa jambo linalowasibu watu wengi kwa pamoja haliwezi kuwa zito kama la mtu mmoja mmoja. Endapo watu watafanya kazi kwa kushirikiana watapata mafanikio kwa urahisi ukilinganisha na yule atakayejitenga na kufanya katika upekee wake. Methali nyingine ni zile ambazo zinawafunza wanajamii kuthamini asili yao pamoja na rasilimali za taifa lao na hivyo kuwajengea ari au moyo wa uzalendo. Nazo kwa kutaja chache ni:

1. 'Funzo la mjinga ni tabu' (uk. 11)
2. 'Radhi ni bora kuliko mali' (uk. 31)
3. 'Mwacha asili ni mtumwa' (uk. 25)

Methali hizi za Kiswahili huwafunza wanajamii kuwa wazalendo kwani hutoa mafunzo yanayowataka wanajamii kuwa na maadili mema katika jamii. Methali isemayo 'funzo la mjinga ni taabu' inawafunza kuwa mtu mjinga na mkaidi siku zote pale inapompata tabu ndipo anapojifunza. Aidha, 'radhi ni bora kuliko mali' inatoa funzo kwa vijana kuwa na adabu na utii ili kupata thawabu kutoka kwa Mwenyezi Mungu na baraka kwa wazazi. Hii ni kwa sababu mali unaweza kuitafuta lakini unapokosa baraka siyo rahisi kuipata tena na hasa mtu unayetarajia kupata baraka kutoka kwake anapokuwa amekufa. Zingine ni zile zinazolenga kufundisha mila desturi na maadili ya jamii. Nazo, kama ambavyo zinaelezwa na Faustine (2017) ni zile zinazoonesha imani ya Waafrika kuhusu umuhimu na thamani ya wazee kwa jamii. Kwa mfano, methali kama 'jungu kuu halikosi ukoko,' 'asiyesikia la mkuu huvunjika guu,' na 'penye wazee hapaharibiki neno', ni zile ambazo zinamjenga kijana kimaadili, na hivyo, kuishi katika misingi sahihi kulingana na mila na desturi za jamii ya Watanzania.

6.0 Hitimisho

Makala hii imeonesha mchango wa lugha ya Kiswahili katika kukuza na kuendeleza uzalendo. Mambo muhimu yaliyojadiliwa ni dhima mbalimbali za lugha ya Kiswahili kwa jamii za Waswahili ambazo zina mchango mkubwa katika kukuza uzalendo na utaifa. Miongoni mwazo ni kutumika kama nyenzo ya mawasiliano ambayo huwezesha kujenga umoja na ushirikiano, kuelimisha, kuhamasisha na pia hutumika kama ghala la kuhifadhia amali mbalimbali za jamii Licha ya dhima zilizojadiliwa, Kiswahili pia kina jukumu kubwa sana kumfanya mtu kuwa huru na hivyo kutoa mawazo yake kwa uhuru katika kukosoa, kuelimisha, kuadilisha na kuhamasisha kwa manufaa ya taifa.

Kutokana na umuhimu huo, ni jukumu la wananchi kuthamini na kuhakikisha wanaitetea lugha ya Kiswahili ndani na nje ya mipaka yao. Wawe mabalozi wazuri katika kuitetea lugha ya Kiswahili kwa masilahi mapana ya taifa. Pia, licha ya juhudi za uhamasishaji wa matumizi ya lugha ya Kiswahili katika shughuli mbalimbali za kiserikali, ni jukumu la serikali kuweka sera hizo katika utekelezaji kwani zimekuwa zikitazamwa kinadharia zaidi bila ya kutekelezwa ipasavyo. Hii itawajengea vijana moyo wa uzalendo na kupata uelewa na utambuzi wa kina kwa kutumia lugha yao ya taifa. Ikumbukwe kuwa ‘mdharau kwao ni mtumwa’ na ‘mcheza kwao hutuzwa.’ Pili, serikali haina budi kuangalia upya lugha inayotumika katika uandishi na utunzaji wa nyaraka mbalimbali ambazo zinayagusa masilahi ya taifa. Miongoni mwa nyaraka hizo ni mikataba ya uwekezaji wa rasilimali za taifa. Kama nyaraka hizo zitaandikwa kwa lugha ya Kiswahili, wananchi wengi wataelewa na hivyo kuweza kutoa maoni yao, kukosoa na kuirekebisha ili kuleta tija kwa taifa.

Marejeleo

- Abdulhamid, M. na Baruwa, A. (2006). *Methali za Kiswahili: Maana na Matumizi Kitabu cha 2*. Dar es Salaam: Mkuki na Nyota Publishers.
- BAKITA, (2017). *Kamusi Kuu ya Kiswahili*. Dar es Salaam. Longhorn Publishers Limited.
- BAKIZA, (2010). *Kamusi la Kiswahili Fasaha*. Nairobi: Oxford University Press.
- Bar, T. na Amos, B. (2004). "Patriotism as a Psycho - Social Phenomenon: Introduction to the Analysis of the Israel Case (Eds.)" Katika *Patriotism*, tel Aviv: Hakibbutz Hameuchad, 13 - 28.
- Cross, S. (2011). *Sociological Theory and Analysis*. London: University of London.
- Faustine, S. (2017). Falsafa ya Waafrika na Ujenzi wa Mtindo wa Uhalisiajabu katika Riwaya ya Kiswahili. Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapwa). Chuo Kikuu cha Dodoma.
- Kasembo, M. J. (2011). *Miaka Hamsini ya Uhuru wa Tanzania Bara: Tulikotoka, Tulipo na Tunakokwenda*. Limuru: Fransiscan Kolbe Press.
- Kezilahabi, E. (1990). *Nagona*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.
- Kothari, C. R. (2004). *Research Methodology: Methods and Techniques*. New Delhi: New Age International (P) Ltd.
- Liundi, C. (2015). *Nukuu za Kiswahili za Mwalimu Julius K. Nyerere: Kutoka kwenye Hotuba na Maandiko*. Dar es Salaam: Mkuki na Nyota Publishers LTD.
- Madumulla, J. S. (2009). *Riwaya ya Kiswahili: Nadharia, Historia na Misingi ya Uchambuzi*. Dar es Salaam: Mture Educational Publishers Limited.
- Mbogo, E. (2015). *Nyerere na Safari ya Kaanani*. Dar es Salaam: Vission Trategic Impact Limited.
- Mohamed, A. S. (1990). *Kivuli Kinaishi*. Nairobi: Oxford University Press.
- _____ (2001). *Babu Alipofufuka*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Mwandosya, M. (2013). *Udhibiti wa Huduma za Kiuchumi Tanzania*. Dar es Salaam: E&D Vision Publishing Ltd.
- REDET, (2005). *Ujenzi wa Imani ya Jamii na Amani Tanzania*. Dar es Salaam: E&D Limited.

- Scott, J. (1995). *Sociological Theory: Contemporary Debate*. Cheltenham: Edward Elgar.
- Senkoro, F.E.M.K. (1987). *Fasihi*. Dar es Salaam: Press and Publicity Centre.
- _____ (1995). Euphrase Kezilahabi: Shaaban Robert wa pili. *Kioo cha Lugha. 1 (1)*, 6169.
- Sewangi, S. S. (2004). "Nafasi ya Lugha katika Maendeleo ya Uchumi: Mfano wa Kiswahili Tanzania" Katika Kihore Y. M na Chuwa, A. R. (Wah), *Kiswahili katika Karne ya Ishirini na Moja*. 87 – 93. Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.
- Simala, I. K. (2017). "Unasibishwaji wa Kiswahili na Taaluma Nyingine kwa Ajili ya Maendeleo" Katika Kandagor, M. et all (Wah), *Lugha na Fasihi katika Karne ya Ishirini na Moja*, 13 - 23. Eldoret: Moi University Press.
- Simiyu, F. W. (2011). *Kitovu cha Fasihi Simulizi*. Mwanza: Serengeti Educational Publishers.
- TUKI, (2004). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Nairobi: Oxford University Press.
- Yonah, Y. (1999). Rousseau and educations towards patriotism. *Politics, Journal of Political Science and International Reletions. 3*, 31-53.